

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

USIMAMIZI BORA WA FEDHA

Biblia inashughulikia swala la pesa, mali, na mielekeo bora ya kifedha ambayo tunastahili kuwa nayo kwa mapana na marefu, hata kuliko somo lingine lote katika Maandiko. Kuna zaidi ya aya 2000 za Maandiko ambazo zinahusiana na swala hili, hasa zinazoguzia maisha yetu ya kifedha na ya kiroho.

Utumizi wa pesa na mali ni kitu cha lazima katika maisha ya kila siku. Fedha ni kitu muhimu katika utimizaji wa wajibu ambao tumepewa na Neno la Mungu kuhusu utunzaji wa familia, kuwasaidia maskini, na hata kusambaza Injili. Kwa sababu swala la kifedha ni jambo muhimu maishani, na kupitia hekima yake isiyo na kipimo, Mungu ametupatia mafundisho muhimu ya kiitikadi, ambayo Mkristo anastahili kufuata, na pia akatupatia kanuni muhimu ambazo zitatusaidia kufaulu katika swala hili la kifedha. Hali ya kifedha ya mtu ni jambo ambalo huadhiri akili na hisia zake, jambo ambalo nalo huadhiri hali yetu ya kiroho; ndiposa ni muhimu kwa Wakristo kuwa na mwelekeo wa kifedha ambao unalingana na Biblia, ili waweze kuwa na uhusiano bora wa kila siku na Mungu, uhusiano ambao unakubalika naye.

Hata ingawa ulimwengu huongozwa na mwongozo usio wa kweli unaosema kwamba kila mwanadamu ana mali ya kibinafsi, mwongozo ambao unazua tamaa, wivu, na watu kutamani mali ya wenzao, mwelekeo wa kibiblia kuhusu mali ya kidunia uko tofauti kabisa na wa ulimwengu. “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi” (Mwanzo 1:1). Vyote vilivyoko ulimwenguni ni vya Mungu na “kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu” (Yakobo 1:17).

Mungu amewakabidhi wanadamu vitu vya maisha haya ili wawe watunzaji wa mali yake

kwa njia ambayo ni ya kuwajibika. Ulimwengu huu ungekuwa tofauti kabisa kama watu wangeelewa kwamba vitu za ulimwengu sio zetu bali ni za Mungu. Sisi ni wasimamizi tu wa vyote tulivyo navyo na maamuzi tunayofanya kuhusiana na fedha yanastahili kuwa ya kutimiza kile ambacho kinamtukuza Mungu. “Kupenda fedha” (1 Timotheo 6:10) ndilo shina moja la “mabaya ya kila namna,” lakini fedha zenyewe hazina shida yoyote. Yesu akasema kwamba “Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; . . . hamwezi kumtumikia Mungu na mali” (Mathayo 6:24). Basi ndio sababu Wakristo wanastahili kuwa waangalifu ili wasiwe watumishi wa mali, na badala yake waruhusu mali kuwatumikia, huku wakitambua kwamba hazina ya kweli haipatikani katika mambo ya ulimwengu huu.

Msimamizi bora na mwenye hekima hufanya maamuzi ambayo si ya kibinafsi bali yale ambayo yanampendeza Bwana wake. Kama wasimamizi wa fedha za Mungu fedha tulizo nazo zinahitaji kuongozwa na kushughulikiwa kwa makini na kwa uaminifu kama kwamba ni jambo la kiroho. “Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu” (1 Wakorintho 4:2).

Yesu mwenyewe aliuliza swali ambalo linafaa sana katika Luka 16:11, “Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli?” Na kama inavyodhihirika katika mfano wa talanta (Mathayo 25:14-30) Wakristo wanastahili kuwa wasimamizi bora na wenye kuaminika wa mali ambayo wamekabidhiwa na Mungu. Usimamizo bora wa fedha ni kwamba mtu atatumia fedha alizo nazo kwa njia ambayo inampendeza Mungu; kwa vile anavyopata fedha hizo, jinsi anavyozitumia, na jinsi ambavyo anaziwekeza na kuzitunza. ■



“Kama wasimamizi wa fedha za Mungu fedha tulizo nazo zinahitaji kuongozwa na kushughulikiwa kwa makini na kwa uaminifu kama kwamba ni jambo la kiroho.”

Thiolojia ya Umaskini
Ikilinganishwa na
Thiolojia ya Utajiri

2

Tahari
Uwezo wa Riba ya
Mchanganyiko

3

Mafundisho ya Biblia:
Usimamizi Bora wa
Fedha

4

Kanuni za Biblia
Kuhusiana na
Usimamizi Bora wa
Fedha 5
Ndoa na Pesa

7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

THIOLOJIA YA UMASKINI IKILINGANISHWA NA THIOLOJIA YA UTAJIRI



Thiolojia ya umaskini na thiolojia ya utajiri ni mafundisho mawili tofauti kuhusu fedha, thiolojia ambazo zinapingana, lakini pia thiolojia ambazo zimefundishwa sana katika ulimwengu wa kidini. Thiolojia hizi mbili ambazo zinapingana hufundishwa kwa kutumia maandiko mengi, lakini maandiko ambayo yamenukuliwa nje ya muktadha

wake, na kunukuliwa nje ya mafundisho ya jumla na ya wastani ambayo yanalingana na Neno lote la Mungu.

Thiolojia ya umaskini inafundisha kwamba utajiri silo jambo linalofaa na kwamba umaskini ni kitu ambacho kinampendeza Mungu. Jambo hili huandamana na wazo kwamba Mkristo akichagua kuwa maskini ni jambo ambalo linafaa sana katika dini. Thiolojia hii ndiyo ambayo imefanya Wakristo wengi kuishi maisha yao katika nyumba za utawa, baada ya wao kuamua kwamba wataishi maisha yao wakiwa maskini. Nguzo za mafundisho haya ni maandiko kama yale ya: “Heri ninyi mlio maskini” (Luka 6:20, 24) na “viuzeni mlivyo navyo” (Luka 12:33). Mtu kuwa na mali huonekana kwamba ni jambo la laana, na kwamba ni kazi ya Mungu (peke yake) kutupatia mahitaji ya kila siku. Lakini ukweli ni kwamba, watu ambao hufuata thiolojia hii huwa na maisha magumu ya kupata mahitaji ya kila siku, na hata wanakosa uwezo wa kusaidia maskini, kwa maana wao wenyewe ni maskini.

Nayo thiolojia ya utajiri (ya afya bora na mali) hudai kwamba ni mapenzi ya Mungu Mkristo kupata baraka za kifedha. Thiolojia hii hutilia mkazo swala la maendeleo ya mtu binafsi, na inasema kwamba haya ndiyo makubaliano ambayo Mungu amefanya na mwanadamu—kwamba ikiwa Mkristo atakuwa na imani na kutii Neno la Mungu, basi Mungu atampatia utajiri wa kiroho na wa kimwili. Nguzo ya thiolojia hii ni maandiko kama yale ya: “Kwa maana, amin, nawaambia, Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali . . . halitakuwako neno lisilowezezana kwenu” (Mathayo 17:20) na “Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea” (Mathayo 21:22). Thiolojia hii hutilia mkazo swala la mtu kuwa na imani ili apate baraka zake Mungu, na kwa msemu mwingine thiolojia hii hujulikana kama “itisha-na udai-hadi upate.” Naye mwandishi mmoja amesema thiolojia hii ni aina ya “Uchawi wa Kikristo.” Ni thiolojia ambayo inatilia mkazo mambo ya ulimwengu huu na kwa makosa kudai kwamba baraka za Mungu huonekana kupitia kwa mtu kupata utajiri.

Thiolojia zote mbili za umaskini na utajiri zina nusu-ya-ukweli. Hakuna kitu ambacho ni cha kiroho sana katika utajiri au umaskini. Mateso sio ishara ya mtu kukosa kutii na utajiri sio ishara ya mtu kumpendeza Mungu. Wakristo kamwe hawastahili kuabudu mali. Badala yake wao wanahitaji kujitolea kufanya matendo mema na makubwa ya ukarimu. Wakristo wanastahili kumtumaini na kumwamini Mungu kwa mambo yote. Wao wanastahili kutafuta uhusiano wao na Mungu, kwa sababu uhusiano huo ni muhimu na unafaa. Lakini wao wasifanye hivyo kwa sababu ya baraka za mali ya ulimwengu huu. Kama wasimamizi wa mali za Mungu Wakristo wanahiti kufuata kanuni ZOTE za biblia, na sio tu kufuata kanuni kadhaa ambazo zinaunga mkono thiolojia ambayo imezinduliwa na mwanadamu mwenzao, aidha iwe ni thiolojia ya umaskini au utajiri. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Fanya bidii kuijua hali ya makundi yako; Na kuwaangalia sana ng'ombe zako. —Mithali 27:23

Somo la robo hii ya mwaka ni kuhusu usimamizi wa fedha ambao unalingana na mafundisho ya biblia. Mimi nimeshangazwa na kiwango cha habari iliyoko katika Neno la Mungu kuhusu somo hili. Ilikuwa ni kazi ngumu kwangu kupunguza somo hili kubwa ili liweze kutoshea katika gazeti hili ndogo. Usimamizi wa fedha ni jambo ambalo limefundishwa kwa kiwango hafifu sana kati ya watu wa Mungu, na matokeo yake ni kuingia kwa madhara ambayo yameingia katika ndoa za watu wengi, na hata hasara ikaingia kwa kazi ya Injili kutokana na watu wa Mungu kufuja mali zao, huku wakifuata usimamizi hafifu wa fedha ambazo wamepata kama Wakristo.

Somo kuhusu pesa ni somo ambalo linahusu watu wote. Hii ni kwa sababu jinsi ambavyo tunasimamia kile ambacho Mungu ametupatia ni jambo ambalo linaadhihi hali yetu ya kiakili na hata jinsi ambavyo tunahusiana na Mungu kwa mambo ya kiroho. Wakristo wengi huwa ni watumishi wa pesa aidha kwa kuwa na madeni mengi au kwa kupenda mali ya ulimwengu huu sana. Ni ombi langu kwamba Mungu atatusaidia ili tuchukulie mali ya ulimwengu huu kwa njia ambayo inafaa maishani mwetu.

Hebu tena niseme kwamba somo hili ni somo muhimu sana. Ni ombi langu kwamba Mungu atabariki habari itakayotolewa kwenye gazeti hili ili msomaji awe na shauku ya kuchunguza zaidi kweli ambazo zinapatikana hapa. Ni jambo moja mtu kuwa na ufahamu kichwani mwake, na ni jambo tofauti kabisa mtu kutumia kanuni hizi maishani mwake. Hebu basi chukua muda kutafakari kuhusu hali yako ya kifedha. Chukua hatua ili kufanya mabadiliko yanayohitaji, na pia uchukue hatua zingine za kujinyima ili kuhakikisha kwamba hali yako ya kifedha iko sawa, na kwamba unafuata kanuni ambazo zinakufaa wakati huu, na hata kwa siku sijazo, ili wewe uweze kuwa mtu wa kuleta baraka kwa watu wale wengine.

Michael W. Smith
Januari 2019



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

NGUVU ZA RIBA YA MCHANGANYIKO

Hakutawahi kuwa na wakati rahisi kwa mtu kuweka akiba na kuwekeza rasilmali. Kuna watu wengi matajiri na maskini ambao wanaamini kwamba hawawezi kupata pesa za kuwekeza. Lakini ukweli ni kwamba watu hawastahili kuishi bila kuwa na akiba na pia bila wao kuwekeza. Kutoka kwa mkulima wa mashambani hadi kwa mfanyi kazi ofisini, wakati ambao unafaa wa kuwekeza ni wakati huu wa sasa, hata ikiwa kiasi cha pesa kinachowekezwa kitakuwa kidogo. Watu wengi wanaweza kuondoa kitu fulani kutoka kwa matumizi yao ya kila siku na kuweka akiba kiasi hicho cha pesa ambacho wangetumia kununua kitu hicho—iwe kwamba ni pesa ya kununua soda au viazi vya kukaanga. Kile ambacho ni kidogo kinaweza kukua na kuwa kikubwa kupitia kwa nguvu za riba ya mchanganyiko. Mtu kuweka kiasi fulani cha pesa bila kukoma kufanya hivyo, hilo ni jambo ambalo litafanya pesa hizo kuongezeka kulingana na jinsi ambavyo wakati unasonga mbele—basi ni vizuri mtu kuanza kuweka akiba yake huku akiwa angali kijana.

Tazama nambari zilizopo hapa (chini) ambazo ni matokeo ya mtu kuweka akiba kiasi fulani kwa miaka arobanne kwa riba ya asilimia 8%.


Kulingana na jinsi ambavyo muda au riba inavyoongezeka ndivyo nambari hizi zitabadilika kwa kiwango kikubwa. Hii ndiyo sababu tunakuomba utambue nguvu za riba ya mchanganyiko.

Kuwekeza shilingi 500 kwa riba ya 8% kwa miaka 40 utapata Ksh. 1,653,700
[Na Kiasi cha Pesa utakachokuwa umetoa mfukoni mwako ni: Ksh. 240,000]

Kuwekeza shilingi 5,000 kwa riba ya 8% kwa miaka 40 utapata Ksh. 16,537,300
[Nacho Kiasi cha Pesa utakachokuwa umetoa mfukoni mwako ni: Ksh. 360,000]

Kuwekeza shilingi 10,000 kwa riba ya 8% kwa miaka 40 utapata Ksh. 33,074,700
[Nacho Kiasi cha Pesa utakachokuwa umetoa mfukoni mwako ni: Ksh. 4,800,000]

Kuwekeza shilingi 100,000 kwa riba ya 8% kwa miaka 40 utapata Ksh. 330,747,000
[Nacho Kiasi cha Pesa utakachokuwa umetoa mfukoni mwako ni: Ksh. 48,000,000]



Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Usimamizi Bora wa Fedha

Somo la Biblia: *Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.* —1 Wakorintho 4:2

Muhstasari: Mafundisho na kanuni za usimamizi wa fedha ni sehemu muhimu ya Agano la Kale na Agano Jipya. Mtoto wa Mungu anastahili kusimamia mambo ya sasa ya mpito kwa uaminifu na ukweli. Ni jambo muhimu Mkristo kufuata mpango unaolingana na Maandiko katika maswala yake ya kifedha, ili yeye aweze kufanya kazi yake, kulipa madeni yake, na kupeana fedha zake, na hata kwa ajili ya kujiandaa kwa siku zake za usoni, wakati ambao yeye ataishi kulingana na jinsi ambavyo Mungu hukutana na mahitaji ya watu wake—jinsi ambavyo Yeye hutunza watu wake.

Maana: Usimamizi Bora — Kusimamia kwa uangali na uwajibikaji kitu ambacho mtu amekabidhiwa kutunza.



I. Usimamizi Bora

- A. Yakobo 1:17 Kila kitolewacho hutoka juu.
- B. 1 Wakorintho 3:9 Wafanyi kazi pamoja na Mungu (1 Wakorintho 4:2).
- C. Luka 16:10-11 Uaminifu kwa mambo ya pesa.
- D. Mathayo 25:14-30 Mfano wa Talanta.

II. Kufanya Kazi kwa Bidii

- A. Warumi 12:11 Si walegevu katika utendaji kazi (Mithali 10:4).
- B. Mithali 24:30-34 Shamba la mtu mlegevu/mvivu.
- C. 2 Wathesalonike 3:10-13 Fanya kazi ili upate chakula chako.

III. Wape Watu Wale Wengine

- A. Matendo 20:35 Ni heri kutoa.
- B. 2 Wakorintho 9:6-7 Kutoa kwa moyo mkunjufu.
- C. Kumbukumbu 16:17 Kutoa kulingana na uwezo wako.

IV. Kutana na Mahitaji ya Familia yako

1 Timotheo 5:8 Tunza watu wa nyumba yako.

V. Ukweli na Uadilifu

- A. Mithali 22:1 Jina jema.
- B. Mithali 22:16 Usiwaonee maskini.
- C. Kumbukumbu 25:13-15 Kipimo kilicho haki.

VI. Lipa Madeni na Uwalipe Wafanyi Kazi Wako

- A. Walawi 19:13 Lipa mishahara ya wafanyi kazi wako (Yeremia 22:13).
- B. Yakobo 5:4 Usimhadai yeyote.

VII. Lipa Ushuru

- A. Mathayo 22:17-21 Mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari.
- B. Warumi 13:7 Lipa kodi na ushuru.

VIII. Deni

- A. Mithali 22:7 Akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.

- B. Warumi 13:8 Usiwe na deni la yeyote.
- C. Zaburi 37:21 Asiye haki hukopa na halipi.
- D. Mithali 22:26-27 Usiwe mdhamini wa deni za watu.

IX. Panga Mambo Yako Vizuri na Uwe na Bajeti

- A. Luka 14:28-30 Hesabu gharama.
- B. Mithali 27:23 Jua hali ya makundi yako.

X. Weka Akiba na Uwekeze

- A. Mithali 6:6-8 Mwendee chungu.
- B. Mithali 21:20 Wenye hekima huweka hazina.
- C. Mwanzo 41:34-36 Yusufu akiwa Misri.
- D. Mathayo 13:44-46 Kununua na kuuza (Mithali 31:16).
- E. Mithali 13:22 Achia wanao urithi.

XI. Maonyo

- A. Mhubiri 5:10 Utajiri hautoshelezi.
- B. 1 Timotheo 6:17-18 Usitumaini utajiri usio yakini.
- C. 1 Timotheo 6:9-10 Kupenda pesa.
- D. Luka 12:15 Tahadhari tamaa ya vitu.
- E. Mathayo 13:22 Udanganyifu wa utajiri.
- F. 1 Yohana 2:15-17 Usiupende ulimwengu.
- G. Marko 8:36 Itamfaidi nini mwanadamu?

XII. Mtumaini Mungu

- A. Mathayo 6:19-33 Mtumikie Mungu, sio pesa, kwa maana Baba yenu anafahamu mnachohitaji.
- B. Wafilipi 4:11-13 Tosheleka (Waebrania 13:5-6).
- C. Wafilipi 4:19 Mungu atakutana na mahitaji yako.
- D. 1 Petro 5:7 Mungu anakushughulikia.

Tamati

Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? —Luka 16:11

KANUNI ZA BIBLIA KUHUSIANA NA USIMAMIZI BORA WA FEDHA

Maandiko yametupatia kanuni nyingi za usimamizi bora wa fedha, kanuni ambazo zimeelezwa kwa njia ya wazi. Kama mtu ataweza kufuata kanuni hizo jambo hilo litamwezesha kupata amani nyingi akilini mwake, na pia kupata hali ya utulivu moyoni.

Kufanya Kazi kwa Bidii

Wakristo wanastahili kuwa watu wenye ari na bidii ya kazi, na kamwe hawastahili kuwa walegevu kazini. Mithali 24:30-34 inaonyesha hali ya shamba la mtu mvivu ambaye hapalili shamba lake. Kutokana na mwelekeo wake wa kutojali na yeye kutokuwa makini, shamba hilo huwa halitoi mavuno mazuri, na kwa hivyo ufukara unamwingia. Wakristo ambao wanafuata kanuni za usimamizi bora huwa na mpango mwema kazini, na pia huwa watu wenye bidii ya kazi. Wao huwa waaminifu kufika kwa wakati wanapowapatia watu wengine miadi ya kukutana nao, na hata biashara



“Wakristo ambao wanafuata kanuni za usimamizi bora huwa na mpango mwema kazini, na pia huwa watu wenye bidii ya kazi. Wao huwa waaminifu kufika kwa wakati wanapowapatia watu wengine miadi ya kukutana nao, na hata biashara ya Mkristo inastahili kufanywa kwa ubora wa hali ya juu.”

(Kumbukumbu 16:17). Hata ingawa utoaji wa fungu la kumi ni fundisho la Agano la Kale matendo ya kuwapatia watu wale wengine ni sehemu muhimu ya usimamizi bora wa fedha. Wasimamizi bora wanastahili kutoa

ya Mkristo inastahili kufanywa kwa ubora wa hali ya juu. Mwelekeo wa kutaka “vya bure” sio mwelekeo unaokubalika na Maandiko. Wathesalonike wa pili 3:10-12 inasema, “Ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula.” Mtume Paulo aliwaamuru watu wale ambao hawakuwa wakifanya kazi kwa sababu ya uzembe “watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe.” Kutoka wakati ambapo Adamu alifanya makosa mwanadamu aliamuriwa kufanya kazi ili ale chakula cha jasho lake, na pia kufanya kazi kwa mikono yake mwenyewe.

Mpe Mungu Kwanza

Wakati umepata mavuno ya shambani, ukilipwa mshahara, ama upate fedha kutokana na juhudi zingine zako, kumbuka kwamba fedha hizo zote ni za Bwana. Msimamizi mwema wa fedha za Mungu huwa hajaribu kushikilia pesa za mwenyewe bali yeye hujaribu kuzitumia kama alivyoagizwa na mwenyewe. Ni mapenzi yake Mungu kwamba wasimamizi wa mali yake wapatiane kwa ukarimu na kwa moyo mkunjufu ili kuunga mkono kazi ya Bwana na hata kuwasaidia maskini. “Kila mtu na atoe kama awezavyo, kwa kadiri ya baraka ya Bwana, Mungu wako, alivyokupa”

kwa moyo mkunjufu na kwa hiari (2 Wakorintho 9:6-7) kwa maana Bwana alisema, “Ni heri kutoa kuliko kupokea” (Matendo 20:35). Kutoa huku kunahitaji kuwe kumetokana na mapato yetu ya kwanza, na ni jambo ambalo linahitaji kufanywa bila kusitasita na kwa nidhamu, bila kujali misukumo mingine ya kifedha ambayo mtu anaweza kuwa nayo wakati tofauti tofauti.

Kutana na Mahitaji ya Familia Yako

1 Timotheo 5:8 imetoa miongozo kuhusu jukumu la mtu kutunza familia yake: “Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.” Hata ingawa Mungu daima anastahili kuwa wa kwanza katika matumizi yetu ya kifedha, mwanaume pia anastahili kutumia pesa zake kukutana na mahitaji ya mke na watoto wake. Mtu ambaye anamkiri Kristo lakini ambaye anatumia pesa zake kwa ajili ya mambo mengine, na kukosa kukutana na mahitaji ya familia yake, ni mbaya zaidi hata kuliko yule ambaye tayari ashamkana Mungu.

Ukweli na Uadilifu

Kuna njia tofauti za kupata pesa lakini mtu anayesimamia pesa kwa njia bora anahitaji kufanya mambo yote, ya kibinafsi na ya biashara yake, kwa ukweli na uadilifu. “Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi” (Mithali 22:1). Kuna watu wengi ulimwenguni ambao hupata pesa kupitia kwa biashara zisizofaa au kwa kuwahadaa watu wale wengine. Lakini hizi sio njia zinazokubaliwa na Biblia. “Yeye awaoneaye maskini ili kuongeza mapato . . . hupata hasara” (Mithali 22:16). Kumbukumbu la Torati 25:13-15 inafundisha kwamba vipimo ambavyo vitatumika vinahitaji kuwa vikamilifu na vya haki. Kwa maneno mengine, kunahitaji kuweko na ukweli katika biashara zote za Mkristo na kamwe yeye hastahili kuwa na njia za kichinichini za kujaribu kudanganya au kuwahadaa watu wale wengine. Njia ndanganyifu za kufanya biashara ni njia za uhakika za Mkristo kudunisha heshima yake, pamoja na kudunisha heshima ya ushirika wa watu wa Mungu.

Lipa Madeni na Wafanyi Kazi Wako

Mwenye kusimamia fedha kwa njia bora (njia ya kiungu) pia huwa hana budi kujitahidi kulipa mishahara na madeni yake kutokana na huduma ambazo amepokea. Yeye anahitaji kuwa mwaminifu kulipa madeni yote kwa wakati unaofaa. Maandiko ya Yeremia 22:13 na Walawi 19:13 yametuonya dhidi ya sisi kuwahadaa majirani zetu kwa kutolipa mishara yao ya huduma na kazi ambazo wametufanyia. Ni tendo la unyang’anyi mtu kumwajiri mwingine kumfanyia kazi, ama mtu kutumia huduma fulani (kama vile stima na maji) na kukosa kulipa madeni hayo. “Angalieni, ujira wa

(Endelea katika Ukurasa 6)

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi” (Yakobo 5:4).

Lipa Ushuru wa Serikali

Hatia nyingi za kisheria zinazofanywa na watu walioajiriwa maofisini, na hata biasharani, ni zile ambazo zimetokana na wao kutolipa ushuru wa serikali. Lakini Biblia imeshughulikia swala hili kwa njia ya wazi kabisa.



“Ni jambo la busasa mtu kuwa na mpango wa kifedha na bajeti ya matumizi, na pia awe na mpango wa kutoa/kupeana na kuweka akiba kulingana na mapato yake.”

Mkristo anayesimamia fedha kwa njia bora hastahili kufanya hivyo. Yesu alisema, “Mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari” (Mathayo 22:21). Kwa kweli Yeye alikuwa akizungumzia haja ya Wakristo kulipa ushuru kwa serikali za dunia. Nayo Warumi 13:7 inaunga mkono swala hili kwa kuwaagiza Wakristo wamlipe “Mtu wa kodi, kodi; mtu wa ushuru, ushuru.”

Mkristo anastahili kulipa kile ambacho Serikali inamwitisha, na ambacho kinalingana na sheria iliyoundwa na serikali hiyo.

Deni

Warumi 13:8 inasema kwamba, “Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana.” Kimuktadha Biblia halikatazi kabisa mtu kuchukua deni, lakini Biblia inafundisha kwamba kama mtu ana deni la kifedha hana budi kulilipa. Lakini deni la upendo ni moja ya deni ambazo kamwe haliwezi kulipwa kabisa. Kuna

maandiko mengi ambayo yanatoa mwongozo kuhusu deni, lakini kamwe maandiko hayo yote hayamkatazi mtu kuwa na deni au kuchukua mkopo. Lakini maandiko yenyewe yametukanya (kwa njia ambayo ni ya wazi kabisa) kuhusu hatari za mkopo. Deni linaweza kufanya mtu kuwa na masumbufu mengi, na pia linaweza kuadhiri furaha na amani ya mtoto wa Mungu. Hii ndiyo sababu mambo ya deni na pesa ni mambo ya kiroho. Zaburi 22:7 inasema kwamba, “Akopaye ni mtumwa wake akopeshayee.” Watu wengi ni watumwa wa deni na wamefungwa na shida nyingi za kifedha. Lakini ni mapenzi ya Mungu kwamba watoto wake wawekwe huru kutokana na utumwa huu. Lakini uhuru kutokana na deni unatokana na mtu kufanya bidii isiyokoma na kufanya juu chini na hata kujinyima ili aweze kulipa madeni yake na ili aweze kuwa huru kutokana na utumwa huo wa kideni. Ikiwa Mkristo anadaiwa pesa na mtu mwingine yeye hana budi kulipa deni hilo bila kujali itachukua muda gani kufanya hivyo. Watu waovu ndio hukopa na kukosa kulipa mkopo wao (Zaburi 37:21).

Deni ni mtego wa Shetani na watu wengi wamepotea kwa sababu ya kufanya maamuzi ya kifedha ambayo hayafai. Wakati mwingi watu huangukia katika madeni kwa sababu ya wao kutumia pesa zaidi ya mapato yao kupitia kwa wao kununua bidhaa ambazo ni za bei ya juu, na ambazo sio za lazima. Kizazi hiki kimeingiwa na msukumo

mkubwa wa kupata vitu kutokana na nia ya kujionyesha, tamaa, na hata wivu wa mtu dhidi ya jirani yake. Hii ndiyo sababu Mkristo anastahili kuwa mwangalifu hasa katika utumizi wa kadi ambazo zinamwezesha kupata vifaa kwa mkopo, na dhidi ya maamuzi wa kuchukua madeni (ya moja kwa moja) ili kupata vitu hivyo kama hivyo. Vijana wengi huwa na shauku ya kuwa na vitu ambavyo baba na mama yao wako navyo bila wao kufanya kazi kwa miaka mingi kama wazazi wao, na ndiposa wao huingia katika madeni ili kupata vitu hivyo. Lakini huu ni mtego wa Shetani na vijana wanahitaji kuwa macho ili wasiingie kwenye tope hilo la deni. Wakati watu wameingia kwenye madeni sio tu kwamba furaha na amani yao inaweza potea lakini pia wao huwa hawana pesa za kutoa kwa hiari kwa kazi ya Bwana. Mungu anatutaka tutumie pesa anazotupatia na kuzisimamia kwa nidhamu na pia ili tuweze kuishi maisha ambayo yanazingatia viwango vya wastani vya maisha. Basi tunahitaji kuishi kwa njia ya mtu wa kawaida hata ikiwa tunao uwezo wa kuishi maisha ya kufurahia vitu vitamu vya maisha haya.

Panga Mambo Yako Vizuri na Uwe na Bajeti

Yesu aliongea kuhusu umuhimu wa mtu kuhesabu gharama kabla ya kujenga mjengo ili isifike mahali ambapo hatakuwa na pesa za kutosha za kumaliza mjengo huo. Katika andiko hili kunapatikna kanuni na somo la kimsingi kabisa kuhusu usimamizi bora wa fedha. Ni jambo la busasa mtu kuwa na mpango wa kifedha na bajeti ya matumizi, na pia awe na mpango wa kutoa/kupeana na kuweka akiba kulingana na mapato yake. Ni jambo la msaada mkubwa ikiwa mtu atakuwa na rekodi ya mapato na matumizi yake na kusimamia rasilimali yake ili awe na usimamizi bora wa kifedha. Lakini watu wengi si waangalifu katika usimamizi wao na hawajui hali yao ya kifedha. “Fanya bidii kuijua hali ya makundi yako; Na kuwaangalia sana ng’ombe zako” (Mithali 27:23). Mtu kuwa na elimu na habari ambayo inafaa ni jambo ambalo litamwezesha kufanya maamuzi bora. Watu wote, wawe matajiri au maskini, wanastahili kuwa na mpango bora wa kifedha na hata bajeti ya matumizi.

Weka Akiba na Uwekeze Pia

Wakati mwingine swala la mtu kuwa na akiba na kuwekeza ni jambo ambalo humfanya mtu kuonekana kwamba hana imani. Lakini Neno la Mungu inafundisha kwa njia iliyo wazi kabisa kuhusu umuhimu wa mtu kuwa na akiba kwa ajili ya siku za usoni. “Ewe mvivu, mwendee chungu, zitafakari njia zake ukapate hekima . . . lakini hujiweke akiba ya chakula wakati wa jua; hukusanya chakula chake wakati wa mavuno.” (Mithali 6:6-8). Maagizo ambayo Mungu alimpatia Farao wa Misri ni yeye kuweka akiba wakati wa mavuno mengi ili kujianda kwa ajili ya wakati wa njaa (Mwanzo 41:34-36). Watu wenye hekima huweka akiba na kukeza kwa sababu wao wanajua kwamba itafika wakati ambapo uzee hautawawezesha kufanya kazi, na mapato yatakuwa ya chini sana. Katika miaka fulani mavuno huwa mengi, na baadaye katika miaka mingine yanakuwa madogo, basi mtu anahitaji kupanga mambo yake vizuri na kuweka akiba ili kujiandaa kwa ajili ya tofauti hiyo ya majira.

Yesu alitoa mfano wa mtu ambaye aliuza kila kitu alichokuwa nacho ili kununua hazina iliyokuwa shambani. Yeye alikuwa akifundisha kanuni ya kifedha ya umuhimu

wa mtu kuwekeza na pia akufundisha somo la kiroho (Mathayo 13:44-46). Yeye pia alitumia wazo kama hilo katika mfano wa talanta ambayo inahadithia jinsi mtu mmoja alificha talanta yake sakafuni na akakosa hata kuiwekeza kwa watu wa kubadilisha fedha ili kupata faida. Ni jambo la busara mtu kuweka akiba na kuwekeza kwa muda mrefu ili kupitia kwa mchanganyiko wa riba pesa nyingi zaidi zitaweza kupatikana kwa ajili ya matumizi ya miaka ambayo mtu hatakuwa na mapato makubwa. Wakati bora sana wa kuweka akiba na kuwekeza ni ule ambao mtu angali kijana. Kwa kweli hakuna mtu ambaye anaweza kukosa njia za kutumia fedha zake, lakini mtu mwenye hekima huendelea kuweka akiba kidogo kidogo cha kiasi fulani cha mapato yake kwa ajili ya siku za usoni.

Maonyo

Hata ingawa pesa ni kitu cha lazima ambacho kinastahili kushughulikiwa kwa njia ya kiungu, Bibla ingali inatoa maonyo mengi kuhusiana na mieleko yetu kuhusu pesa. Utajiri haumtoshenzi mwanadamu (Mhubiri 5:10) na Mkristo kamwe hastahili kuweka tumaini lake katika “utajiri usio yakini bali wamtumaini Mungu” (1 Timotheo 6:17-18). Hata ingawa Wakristo wanahitaji kufuata njia bora za usimamizi wa fedha, lakini mioyo na upendo wao haustahili kuwa ni kwa utajiri wa ulimwengu huu wala kufuata mambo ya dunia hii (1 Yohana 2:15-17). “Jilindeni na choyo” (Luka 12:15) na tutambue kwamba utajiri unaweza kumhadaa mtu na kufanya Neno la Mungu lisikue ndani ya Mkristo (Mathayo 13:22). Hazina ya kweli hupatikana ndani ya Yesu Kristo na Yeye ndiye anastahili kudumu katikati mwa makusudio yetu na malengo yetu ya maisha haya. “Kwa kuwa itamfaida mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?” (Marko 8:36).

Ndoa na Pesa

Utafiti unaonyesha kwamba pesa ni moja ya sababu kubwa zinazofanya ndoa kuwa na shida na ni moja ya sababu kuu ya watu kufanya talaka. Maswala ya kifedha yanaweza kuwa changamoto kubwa nyumbani lakini changamoto kama hizo zinaweza kupunguzwa kwa waliooana kufuata kanuni zinazofundishwa na biblia.

Katika Mathayo 19:6 Yesu alikuwa akizungumza kuhusu ndoa na kusema kwamba mke na muume sio miili miwili tena bali wao ni mwili moja. Lakini jambo hili halihusiani tu na mambo ya kimwili ya mume na mke katika ndoa. Ndoa ni jambo ambalo linahusisha umoja wa pamoja, na jambo hilo pia linahusika kwa mambo ya kifedha. Hata ingawa sisi tunaheshimu tofauti za tamaduni mbali mbali ndoa huwa na nguvu zaidi wakati mambo ya kifedha yanafanywa kwa pamoja. Kuna shida ambayo huzuka katika ndoa ikiwa wahusika watakuwa na vitu vyao vya kibinafsi, ambavyo kila mmoja anasimamia bila kumhusisha mwenzake. Ni bora zaidi wale walioona kutengeneza pesa ambazo ni zao kwa pamoja, watumie pesa pamoja, wawekeze kwa pamoja n.k. Ikiwa mmoja wa washiriki wa ndoa atakuwa na kasumba kwamba ni lazima awe ni yeye “wa kupewa,” jambo



Mtumaini Mungu

Wakristo hawastahili kutumaini mambo ya ulimwengu huu bali wanahitaji kumtumaini Mungu ambaye yuko hai. Baba yetu wa mbinguni anajua kile tunahitaji, na Yeye huwatumia watoto wake (Mathayo 6:19-33). Hata ingawa jambo hili si kusema kwamba mtu asifuate kanuni bora za kifedha, moyo na mielekeo ya akili za Mkristo kuhusiana na pesa unahitaji kuwa tofauti kabisa na mielekeo ya watu wa ulimwengu huu. Mkristo anastahili kutambua kazi na wajibu ambao pesa na mali zinahitaji kuwa nao katika maisha yake huku akidumisha tumaini na imani yake kwa Mungu. Mtoto wa Mungu anahitaji kujifunza kuwa na mwelekeo wa kutosheleka (Wafilipo 4:11-13) na awe na amani moyoni huku akijua kwamba “Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.” (Wafilipi 4:19).

Ni ombi letu kwamba Mungu atabariki kila mtoto wake ili aweze kuzingatia masomo na hekima ya kanuni hizi za biblia zinazohusiana na usimamizi bora wa kifedha. Kuna wale ambao wamepuuza kanuni hizi aidha kwa kufuata mambo ya ulimwengu, na wengine kwa kufuata mambo ya utakatifu, na mwishowe wakaingia hasara ya kiroho na kifedha. Hata ingawa umaskini au utajiri si ishara ya hali ya kiroho ya mtu, vile ambavyo mtu husimamia fedha zake ni jambo ambalo linadhahirisha utiifu wake kwa Neno lake Mungu. Kuna baraka kubwa ambayo inamsubiri yeyote ambaye atafuata Maandiko yanayohusiana na swala hili. Je, kama sisi sio waaminifu kwa pesa na kwa mambo ya ulimwengu (huu) itawezekanaje Mungu kutuamini na kutupatia utajiri wa kweli wa ufalme wa Mungu? (Luka 16:11). ■

hilo linaweza kuleta kinyongo katika uhusiano wao.

Ni bora zaidi ikiwa maamuzi ya mambo ya kifedha yatafanywa kwa pamoja. Na mtu kuzungumza na mwenzake ni moja ya njia muhimu ya kupunguza masumbufu ya pesa katika ndoa. Watu kuwasiliana kwa uwazi kuhusu hali halisi ya kifedha iliyopo hapo nyumbani ni jambo muhimu ikiwa wao wataweza kufanya mambo yao kwa pamoja. Na ikiwa waliooana watakuwa na bajeti na mpango bora wa kifedha hili litakuwa ni jambo litakalosaidia kupunguza masumbufu ambayo yanaweza kuwoko wakati wawili hawa wanaanza kulaumiana kwa jinsi ambavyo kila mmoja wao anatumia pesa. Ni muhimu wao wajadili tabia za kifedha za kila mmoja wao, na kusiwe na mtu wa kujisikia kwamba anaingiliwa; basi wanahitaji kujadili mambo haya kwa neema na heshima, huku wakitambua kwamba wahusika wa ndoa wanaweza kuwa na mielekeo tofauti kuhusu pesa. Mume na mume wanastahili kutambua wajibu na kazi muhimu (lakini ambayo ni tofauti) ambayo kila mmoja wao hufanya pale nyumbani; lakini pia wao wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya manufaa ya kifedha ya wote wawili ili wasipatwe na masumbufu ya kiakili kutokana na maswala ya kifedha. ■



JE, WAJUA?

Deni Linalofaa Likilinganishwa na Deni Lisilofaa

Madeni yote hayafanani. Inasemekana kwamba deni linalofaa ni lile ambalo linasaidia kuleta mapato na pia kuongeza thamani ya mtu kama vile elimu, kuwa na biashara, kuwa na mijengo, na pia uwekezaji. Lakini kwa kweli hata deni “linalofaa” halina uhakika na hata nalo linaweza kumletea mtu hasara. “Deni lisilofaa” ni lile ambalo linatumiawa kununua vitu ambavyo thamani yake inapungua kama vile magari, nguo, vitu vya kula, na vifaa na huduma zingine ambazo watu hujirimbikiza. Deni ambazo watu wa vyeo fulani katika jamii huchukua kwa njia ya kutumia kadi za kununua vitu katika madukani makubwa ni moja ya deni ambazo zina riba kubwa zaidi, hasa kama madeni hayo hayalipwi kikamilifu wakati mwisho wa mwezi unapofika. ■



MUNGU AJUA MWAHITAJI HAYA YOTE

Tule nini? . . . Au Tuvae nini? . . . kwa sababu Baba yetu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. —Mathayo 6:31-33

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Mara nyingi watumishi wa Mungu ambao wanafanya kazi ya kueneza injili (kama kazi yao ya kila siku) watapitia shida za kifedha na hata wakati mwingine wataingia katika hali ya umaskini huku wakiwa wangukiwa wanajikaza kisabuni kueneza utajiri wa Kristo, badala ya kufuata utajiri wa kidunia. Lakini hata ingawa muda wao na pia vipawa vyao vinahitaji kutumika katika uenezaji wa ufalme wa Mungu, ukweli ni kwamba, pesa ni kitu cha lazima wakati sisi tunaishi ulimwenguni huu. Mungu kwa kweli anafahamu ukweli huu na kamwe hatawasahau watumishi wake wakati wa mahitaji. Watumishi wa injili wanastahili kuwa tayari kuteseka huku wakidumisha imani yao ambayo haitegingisiki, imani ya kuamini kwamba Mungu amewaahidi kuwapa vitu vyote ambavyo ni vya lazima maishani. Na wakati ambapo tunapitia wakati mgumu ndipo wakati imani yetu inahitaji kukua zaidi ya hali iliyopo, na kutambua kwamba Mungu ana kusudi na mpango ambao ni mkuu zaidi.



Maneno ya mtume Paulo ambayo yako katika Wafilipi 4:11-13 yanahitaji kuwa himizo kwetu sote: “Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” Tayari Mungu amekuonyesha kwamba anakupenda na anakujali, na kamwe Yeye hatakuacha ikiwa utadumu huku ukiwa mwaminifu katika kazi yake na kuishi maisha yako kwa ajili ya utukufu wake.

Lakini imani kamwe haidunishi kanuni zingine za Mkristo, kwamba anahitaji kuwa msimamizi bora wa fedha. Haijalishi huduma yako inapata kipato kiasi gani ni muhimu kwa huduma zote kufuata kanuni bora za usimamizi wa kifedha. Wahudumu wa injili wanahitaji kuweka akiba kwa ajili ya siku za usoni kama wanavyofanya watu wale wengine, hata ingawa hatuhitaji kuweka imani yetu katika utajiri usiotegemeka. Basi wewe usiangukie mtego wa kutumia fedha zote sasa kwa kufuja mali yako huku ukitarajia kwamba Mungu atakutunza kesho. Huenda Mungu anakubariki leo ili uweze kuweka akiba ya fedha zako na ndiposa uwe na pesa za matumizi mwezi ambao unakuja.

Mungu ambaye ni baba yetu wa mbinguni anajua shida ambazo uko nazo na pia masumbufu ya kifedha ambayo unaweza kuwa nayo hasa kuhusiana na maslahi ya familia yako. Lakini wewe mtumishi wa Mungu endelea kudumisha imani yako katika Kristo na usiache mwito wako wa kuhubiri injili kwa ajili ya mali ya maisha haya ya sasa. Mungu atakuwa mwaminifu kwa Neno lake na atakuhudumia kulingana na mahitaji yako. ■